



## WAKALA WA VIPIMO TANZANIA

**Zijue njia zinazotumiwa na Wakala wa Vipimo katika kushughulikia malalamiko yako;**

Wakala wa Vipimo ni Taasisi ya Serikali iliyo chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na jukumu lake kuu ni kumlinda mlaji kupitia matumizi sahihi ya vipimo. Ili kuboresha huduma zake;

- Wakala wa Vipimo hupokea malalamiko kupitia njia mbalimbali kama vile barua, madodoso (kwenye maonesho), simu, barua-pepe, mtandao, magazeti, redio, luninga na ana kwa ana.
- Malalamiko huweza kupokelewa na mtumishi yeoyote ndani ya taasisi halafu yanapelekwa masijala na kuelekezwa kwa maafisa malalamiko ili yaweze kushughulikiwa kwa utaratibu ufuatao:-
  - (i) Hupokelewa na kuchambuliwa (nini kimelalamikiwa au nani amelalamikiwa);
    - Malalamiko yaliyopokelewa kama yanahusu taasisi nyingine yanaelekezwa kwenye taasisi husika na kama ni ya taasisi yetu yanaandikishwa na kama yanamajibu ya moja kwa moja Afisa Malalamiko atamjibu/ atampa suluhu mteja.
    - Kama malalamiko hayo hayana majibu/ suluhu ya moja kwa moja yanaelekezwa kwenye Idara husika kwa ajili ya kupatiwa ufumbuzi.



**Afisa Malalamiko akiwaeleza wananchi jinsi malalamiko yanavyoshughulikiwa**

- (ii) Ufumbuzi ukipatikana, Mkuu wa Idara husika atamjibu mteja na kumpa mrejesho kwa Afisa malalamiko;
- (iii) Ufumbuzi wa mrejesho visipopatikana kwa mteja na Afisa Malalamiko, Mkuu wa Idara husika atakumbushwa tena na Afisa Malalamiko;
- (iv) Mkuu wa Idara husika akitoa jibu/ ufumbuzi atampa majibu mteja na mrejesho kwa Afisa malalamiko;
- (v) Endapo Mkuu wa Idara husika atashindwa kutoa ufanuzi taarifa itapelekwa kwa Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Vipimo kwa hatua zaidi;

“Ewe mwananchi! Usikubali kudhulumiwa kupitia matumizi ya vipimo visivyo sahihi, toa taarifa kwenye ofisi zetu zinazopatikana kwa kila Mkoa Tanzania Bara ili ufumbuzi wa lalamiko lako liweze kutatuliwa”

**Kwa maelezo zaidi, wasiliana na;**

Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu, Wakala wa Vipimo,  
S.L.P 313, Dar es Salaam. Simu: +255 (022) 2928156,  
Barua pepe: [info@wma.go.tz](mailto:info@wma.go.tz), Tovuti: [www.wma.go.tz](http://www.wma.go.tz)